# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1003

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-786-9

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA KISWAHILI ELIMU YA SEKONDARI

# KIDATO CHA I–IV

# 2023

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza, 2023

ISBN:978-9987-09-786-9

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S. L. P. 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255-735041168/ +255-735041170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). Muhtasari wa Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha kutafsiri wala kutoa muhtasari huu au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania

## Yaliyomo


Orodha ya majedwali ........ iv

Vifupisho ........ v

Shukurani ........ vi

1.0 Utangulizi ........ 1

2.0 Malengo Makuu Elimu ya Elimu nchini Tanzania ........ 1

3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I-IV ........ 2

4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Sekondari Kidato cha I-IV ........ 3

5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 3

6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 4

6.1 Mwalimu ........ 4

6.2 Mwanafunzi ........ 6

6.3 Mzazi/Mlezi ........ 6

7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 7

8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 7

9.0 Upimaji ........ 7

10.0 Idadi ya Vipindi ........ 8

11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 8

Bibliografia ........ 50

## Orodha ya Majedwali


Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Kidato cha I–IV ........ 3

Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati ........ 8

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Kidato cha I ........ 9

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Kidato cha II ........ 19

Jedwali Na. 5: Maudhui ya Kidato cha III ........ 27

Jedwali Na. 6: Maudhui ya Kidato cha IV ........ 43

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |

# Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu, pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, TET inaishukuru kwa dhati Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwaandaa wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la Uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Dkt. Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Kiswahili ni moja kati ya masomo ya lazima katika ngazi ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV kwa wanafunzi walioko katika Mkondo wa Elimu ya Jumla na Amali. Somo hili linalenga kuendelea kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kuwasiliana kwa ufasaha kwa kutumia lugha ya Kiswahili ambalo ni moja kati ya malengo makuu ya elimu nchini Tanzania na ni moja kati ya stadi za Karne ya 21. Aidha, somo hili linalenga kumwezesha mwanafunzi kumudu Kiswahili, kukitumia na kukithamini. Katika somo hili mwanafunzi atajifunza umahiri mbalimbali ikiwemo kuhariri, kukalimani na kutafsiri na hivyo kuweza kutumia ujuzi huu kumudu maisha yake ya kila siku.

Muhtasari wa Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV umeandaliwa kwa kuzingatia Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV wa Mwaka 2023 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muhtasari huu ni mwendelezo wa Muhtasari wa Elimu ya Msingi Darasa la III–VI na umeendelea kuzingatia mkabala wa kimawasiliano ambao unasisitiza kukuza stadi nne za lugha ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Vilevile, muhtasari unatoa nafasi kwa mwalimu kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Hivyo, muhtasari huu umesisitiza ujenzi wa umahiri wa lugha ya Kiswahili katika mawasiliano mbalimbali.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu nchini Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV

Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV - Elimu ya Jumla ni:

(a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi na mwelekeo alioupata katika hatua ya elimu ya msingi;

(b) Kulinda mila na desturi, umoja wa kitaifa, tunu za taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;

(c) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, na kiufundi;

(d) Kuimarisha mawasiliano kwa kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja nyingine ya kigeni;

(e) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia na utunzaji endelevu wa mazingira;

(f) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na

(g) Kukuza utayari wa kujiendeleza na mafunzo ya elimu ya kati na ya juu.

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV

Umahiri wa jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV - Elimu ya Jumla ni:

(a) Kutumia maarifa na stadi alizozipata katika hatua ya elimu ya msingi kuimarisha na kupanua uelewa wa kitaaluma;

(b) Kuthamini uraia na tunu za taifa;

(c) Kuonesha kujiamini katika kujifunza nyanja mbalimbali zikiwemo Sayansi na Teknolojia, maarifa ya kinadharia na kivitendo;

(d) Kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja nyingine ya kigeni kuwasiliana;

(e) Kutumia maarifa ya masuala mtambuka kuyamudu mazingira yanayomzunguka; na

(f) Kutumia ujuzi na stadi kumwezesha mwanafunzi kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha na mazingira.

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa Kidato cha I–IV umebainishwa katika Jedwali Na.1.

**Jedwali Na 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Kidato cha I–IV*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu misingi ya Kiswahili | 1.1 Kutambua Kiswahili kama kielelezo cha utaifa na utambulisho wa Mtanzania<br>1.2 Kukuza uelewa wa sarufi ya Kiswahili |
| 2.0 Kumudu lugha ya mazungumzo na ya maandishi | 2.1 Kusikiliza na kuelewa mazungumzo<br>2.2 Kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 3.0 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 3.1 Kutumia kamusi katika miktadha mbalimbali<br>3.2 Kuwasiliana kwa ufasaha kwa njia ya mazungumzo<br>3.3 Kuwasiliana kwa njia ya maandishi katika miktadha mbalimbali |
| 4.0 Kuthamini kazi za fasihi ya Kiswahili | 4.1 Kukuza uelewa wa misingi ya fasihi ya Kiswahili<br>4.2 Kuhakiki kazi za fasihi ya Kiswahili<br>4.3 Kubuni kazi za fasihi ya Kiswahili |
| 5.0 Kutoa huduma ya lugha ya Kiswahili katika jamii | 5.1 Kufanya tafsiri sahili katika lugha ya Kiswahili<br>5.2 Kuhariri matini mbalimbali za Kiswahili<br>5.3 Kufanya ukalimani sahili kwa lugha ya Kiswahili |

## 6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

### 6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika somo la Kiswahili;

(b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai, na uwezo wa mwanafunzi ili kumwezesha mwanafunzi:

(i) Kujenga umahiri unaohitajika katika Karne ya 21; na

(ii) Kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji;

(c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali. Mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na; kazi za vitendo, utafiti, majaribio ya kisayansi, majadiliano na kazimradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha, mwalimu anahimizwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa;

(d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;

(e) Kutengeneza au kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;

(g) Kuhakikisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;

(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;

(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;

(j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;

(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 6.2 Mwanafunzi

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri unaokusudiwa; na

(c) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktabamtandao.

### 6.3 Mzazi/Mlezi

Mzazi/ Mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;

(b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;

(c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;

(d) Kufuatilia mwenendo wa tabia ya mtoto;

(e) Kumpatia mtoto vifaa vyote vinavyohitajika katika ujifunzaji;

(f) Kuhakikisha mtoto anapata mahitaji muhimu; na

(g) Kumfundisha mtoto kuhusu umuhimu na thamani ya elimu pamoja na kumuhimiza kujifunza kwa bidii.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni msingi katika kujenga umahiri kwa mwanafunzi. Muhtasari huu umependekeza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila shughuli. Miongoni mwa mbinu hizo ni ziara za kimasomo, kazi za vitendo na kazimradi. Hata hivyo, mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana mbadala zinazopatikana katika mazingira ya shuleni na nyumbani pindi zinapohitajika. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kwa ajili ya rejea vitatolewa na TET.

## 9.0 Upimaji

Upimaji ni mchakato muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Kiswahili. Mwalimu anashauriwa kuwa na uwanja mpana wa uchaguzi wa mbinu na zana za upimaji ili kupima uwezo wa mwanafunzi katika kuwasiliana kwa ufasaha kwa kutumia Kiswahili. Zana zinazoweza kutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ni bunguabongo, orodhahakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi, mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo. Aidha, upimaji utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Hivyo, upimaji endelevu utachangia asilimia 30 ya upimaji wote na upimaji tamati wa kuhitimu Kidato cha Nne utachangia asilimia 70. Mgawanyo wa alama hizi unaoneshwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na 2:** *Alama za Upimaji Endelevu na Tamati*

| Upimaji | Alama (%) |
|---|---|
| Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Sita | 5.0 |
| Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili | 6.0 |
| Mtihani wa muhula wa mwisho wa Kidato cha Tatu | 5.0 |
| Kazimradi inayofanyika mwishoni mwa Kidato cha Tatu | 7.0 |
| Mtihani wa utamilifu wa Kidato cha Nne | 7.0 |
| Mtihani wa kuhitimu Kidato cha Nne | 70 |
| **Jumla** | **100** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Kiswahili Sekondari Kidato cha I–IV unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio haya yamewekwa kwa mfumo wa vipindi, ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vinne (4) kwa wiki kwa kidato cha I–IV.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ufundishaji

Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji yamepangiliwa katika jedwali lenye vipengele saba, ambavyo ni; umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa, vigezo vya upimaji, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa pamoja na idadi ya vipindi. Maudhui hayo yameoneshwa katika Jedwali Na. 3–6.

## Kidato cha I

**Jedwali Na 3:** *Maudhui ya Kidato cha I*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu misingi ya Kiswahili | 1.1 Kutambua Kiswahili kama kielelezo cha utaifa na utambulisho wa Mtanzania | (a) Kutumia Kiswahili katika mijadala mbalimbali kwa kuzingatia utamaduni wa Mtanzania (*mf. matumizi ya tafsida na uteuzi wa maneno kulingana na mila na desturi za Mtanzania*) | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadiliana masuala mbalimbali yanayohusu utamaduni wa Mtanzania katika matumizi ya lugha ya Kiswahili<br>**Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kufanya mdahalo kwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia masuala ya kiutamaduni | Kiswahili kama kielelezo cha utaifa na utambulisho wa Mtanzania kimetumiwa | Matini, video zenye matumizi ya lugha kulingana na utamaduni wa Mtanzania, vitu halisi | 8 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kukuza uelewa wa sarufi ya Kiswahili | (a) Kusimulia habari na matukio kwa kuzingatia kiimbo, mkazo, na lafudhi pamoja na dhima zake | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusimulia visa au matukio mbalimbali kwa kuzingatia kiimbo, mkazo, lafudhi pamoja na dhima zake | Habari na matukio vimesimuliwa kwa kuzingatia kiimbo, mkazo, lafudhi na dhima zake | Kinyonyi chenye mazungumzo yaliyorekodiwa, matini za sarufi, kamusi, chati ya tungo | 36 |
| | | (b) Kuandika hadithi kwa kuzingatia mpangilio na uhusiano sahihi wa maneno (*nomino, vivumishi, vielezi, viwakilishi, vitenzi, vihisishi, vihusishi na viunganishi*) katika sentensi | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini zenye aina mbalimbali za maneno, kisha wabainishe uhusiano wa maneno yanayofuatana katika sentensi, na waandike hadithi kwa kuzingatia mpangilio na uhusiano sahihi wa maneno | Hadithi zimeandikwa kwa kuzingatia mpangilio na uhusiano sahihi wa maneno katika sentensi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuandika hadithi kwa kuzingatia mpangilio na uhusiano sahihi wa sentensi katika aya | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini mbalimbali kisha wabainishe uhusiano sahihi wa sentensi katika aya, na waandike hadithi kwa kuzingatia mpangilio na uhusiano sahihi wa sentensi katika aya<br>**Kazimradi:** Waelekeze wanafunzi kutembelea maktaba na kusoma hadithi mbalimbali kwa kuzingatia mpangilio sahihi wa sentensi, kisha waandike hadithi kwa kuzingatia mpangilio na uhusiano sahihi wa sentensi katika aya | Hadithi zimeandikwa kwa kuzingatia mpangilio na uhusiano sahihi wa sentensi katika aya | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumudu lugha ya mazungumzo na ya maandishi | 2.1 Kusikiliza na kuelewa mazungumzo | (a) Kusikiliza mazungumzo changamani na kujibu maswali | **Ziara:**<br>Wanafunzi watembelee maeneo mbalimbali yenye mazungumzo changamani, kisha wajibu maswali kutokana na mazungumzo waliyoyasikiliza<br><br>**Maswali na majibu:**<br>Waongoze wanafunzi kujibu maswali mbalimbali kutokana na mazungumzo changamani waliyoyasikiliza | Mazungumzo changamani yamesikilizwa na maswali yamejibiwa | Kinyonyi kilichohifadhiwa mazungumzo changamani yaliyorekodiwa | 24 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza kwa muhtasari mazungumzo changamani aliyoyasikiliza | **Majadiliano**: Kuwaongoza wanafunzi kujadiliana katika vikundi kuhusu mazungumzo changamani waliyoyasikiliza, kisha waeleze kwa muhtasari | Mazungumzo changamani aliyoyasikiliza yameelezwa kwa muhtasari | | |
| | | (c) Kushiriki katika majadiliano ya masuala mbalimbali kwa kuzingatia sifa za lugha ya mazungumzo (*mf. lugha ya mkato, kupeana nafasi*) | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kushiriki majadiliano ya masuala mbalimbali kwa kuzingatia sifa za lugha ya mazungumzo | Wanafunzi wameshiriki katika majadiliano ya masuala mbalimbali kwa kuzingatia sifa za lugha ya mazungumzo | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu | (a) Kusoma matini fupi changamani kwa kuzingatia alama za uandishi, kasi sahihi na kiimbo cha tungo | **Michezo:** Waongoze wanafunzi kukaa katika makundi mawili ya ushindani kisha wasome matini fupi changamani kwa kupokezana kwa kuzingatia alama za uandishi, kasi sahihi na kiimbo cha tungo | Matini fupi changamani zimesomwa kwa kuzingatia alama za uandishi, kasi sahihi na kiimbo cha tungo | Matini za kusoma, kadi za maneno/ tungo | 32 |
| | | (b) Kueleza namna alama za uandishi na kiimbo vinavyoathiri ujumbe katika usomaji wa matini fupi changamani | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi changamani, kisha wabainishe umuhimu wa alama za uandishi na kiimbo katika kutoa maana | Namna alama za uandishi na kiimbo vinavyoathiri ujumbe katika usomaji wa matini fupi changamani imeelezwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuandika hoja kuu kutoka katika matini fupi changamani alizozisoma kwa kuzingatia sifa za lugha ya maandishi (*mf. alama za uandishi, miunganiko sahihi ya tungo, usanifu*) | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika jozi kusoma matini, kisha waandike mawazo makuu kwa kuzingatia sifa ya lugha ya maandishi | Hoja kuu kutoka katika matini fupi changamani alizozisoma zimeandikwa kwa kuzingatia sifa za lugha ya maandishi | | |
| | | (d) Kutumia TEHAMA kutafuta maana ya maneno mapya kutoka katika matini aliyoisoma | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kutafuta maana za maneno kwa kutumia vifaa vya TEHAMA | TEHAMA imetumika kutafuta maana za maneno mapya kutoka katika matini aliyoisoma | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 3.1 Kutumia kamusi katika miktadha mbalimbali | (a) Kutumia msamiati kwa usahihi katika mazungumzo na maandishi | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi vidogovidogo wasome kamusi kisha wabainishe taarifa za kikamusi | Msamiati katika mazungumzo na maandishi umetumiwa kwa usahihi | Kamusi na matini za kusoma | 16 |
| | | (b) Kutumia taarifa mbalimbali za kamusi katika mawasiliano ya mazungumzo na maandishi | **Usomaji wa matini:** Andaa maneno mbalimbali kisha waongoze wanafunzi katika vikundi kutafuta taarifa za maneno hayo katika kamusi halafu wayatumie kuwasiliana katika mazungumzo na maandishi | Taarifa mbalimbali za kamusi zimetumiwa katika mawasiliano ya mazungumzo na maandishi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kujibu maswali mbalimbali yanayohusiana na kamusi | | | |
| | 3.2 Kuwasiliana kwa ufasaha kwa njia ya mazungumzo | (a) Kuzungumza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali (*mf. nyumbani, shuleni na hospitalini*) | **Igizodhima:** Waongoze wanafunzi kuigiza nafasi mbalimbali za uhusika katika mazungumzo katika miktadha mbalimbali | Kuzungumza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali kumezingatiwa | Video na kinyonyi kilichohifadhiwa mazungumzo ya mada mbalimbali | 16 |
| | | (b) Kutumia lugha kwa ufasaha katika malumbano ya hoja | **Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kufanya mdahalo | Lugha imetumika kwa ufasaha katika malumbano ya hoja | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kusikiliza vipindi vya redioni au kwenye televisheni kisha waoneshe namna lugha fasaha inavyotumika katika kujenga na kupinga hoja | | | |
| | 3.3 Kuwasiliana kwa njia ya maandishi katika miktadha mbalimbali | (a) Kujieleza kwa ufasaha kwa maandishi katika miktadha mbalimbali | **Kuandika na kuwasilisha:** Wape wanafunzi mada mahususi waandike kuhusu mada hiyo kisha wawasilishe darasani | Kujieleza kwa ufasaha kwa maandishi katika miktadha mbalimbali kumetendeka | Matini za kuandika, picha na michoro, chati za miundo mbalimbali ya uandishi | 8 |

## Kidato cha II

**Jedwali Na 4:** *Maudhui ya Kidato cha II*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu misingi ya Kiswahili | 1.1 Kukuza uelewa wa sarufi ya Kiswahili | (a) Kuandika habari kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi (*kwa kuzingatia ngeli za nomino na viambishi vya upatanisho*) | **Kuandika na kuwasilisha:** Waongoze wanafunzi kuandika kuhusu habari fulani na kuwasilisha darasani ili kubaini uzingativu wa upatanisho wa kisarufi<br>**Ziara:** Wanafunzi wafanye ziara eneo fulani mahususi kisha waandike kuhusiana na tukio walilolisikia au kulishuhudia kwenye ziara hiyo kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi | Habari imeandikwa kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi | Chati za maneno/ tungo, matini za sarufi | 40 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuzungumza kwa kutumia miundo changamani ya sentensi katika miktadha mbalimbali (*sentensi ambatani na changamani*) | **Igizodhima:** Waongoze wanafunzi kuigiza kuhusu mada fulani inayoruhusu kujenga hoja na kutumia miundo changamani ya sentensi | Miundo changamani ya sentensi imetumiwa katika mazungumzo kulingana na miktadha mbalimbali | | |
| | | (c) Kuandika matini fupi kwa kutumia miundo changamani ya sentensi | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini mbalimbali zenye miundo changamani, kisha wabainishe miundo hiyo na kuitumia kuandika matini fupi | Matini fupi zimeandikwa kwa kutumia miundo changamani ya sentensi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumudu lugha ya mazungumzo na ya maandishi | 2.1 Kusikiliza na kuelewa mazungumzo | (a) Kusikiliza habari changamani kwa umakini, udadisi na kuuliza maswali | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi wasikilize habari changamani kwa umakini na udadisi ili kuelewa mazungumzo<br><br>**Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kujibu maswali kutokana na habari changamani waliyoisikiliza | Habari changamani zimesikilizwa kwa umakini, udadisi na maswali yameulizwa | Video na kinyonyi kilichohifadhiwa mazungumzo mbalimbali | 24 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kusikiliza mijadala/ habari changamani na kuwasilisha mawazo makuu aliyoyapata kwa kuzingatia uwazi na uwekevu | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kusikiliza mijadala/ habari changamani kisha wajadiliane na kuwasilisha mawazo makuu waliyoyapata kwa kuzingatia uwazi na uwekevu<br>**Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusimulia habari changamani kisha kuwasilisha mawazo makuu waliyoyapata kwa kuzingatia uwazi na uwekevu | Mijadala/habari changamani zimesikilizwa na mawazo makuu aliyoyapata yamewasilishwa kwa kuzingatia uwazi na uwekevu | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu | (a) Kusoma matini ndefu changamani kwa kina na utunduizi | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini ndefu changamani kwa kina na utunduizi kisha waeleze mambo makuu yaliyomo katika matini hizo | Matini ndefu changamani zimesomwa kwa kina na kwa utunduizi na mambo makuu yaliyomo yameelezwa | Matini changamani za kusoma, kadi za maneno/ tungo | 24 |
| | | (b) Kusoma matini ndefu changamani, kuandika muhtasari wa hoja kuu zilizomo na kutoa maoni juu ya hoja hizo | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini ndefu changamani kisha waandike muhtasari wa hoja kuu zilizomo na kutoa maoni juu ya hoja hizo | Matini ndefu changamani zimesomwa, muhtasari wa hoja kuu zilizomo umeandikwa na maoni juu ya hoja hizo yametolewa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 3.1 Kuwasiliana kwa ufasaha kwa njia ya mazungumzo | (a) Kuzungumza kwa kutumia mitindo mbalimbali ya lugha ya mazungumzo na kwa kuzingatia miktadha, umri, jinsia na uhusiano | **Igizodhima:** Waongoze wanafunzi kuigiza kwa kuzingatia uhusika fulani kulingana na muktadha wa tukio, umri, jinsia na uhusiano | Mitindo mbalimbali ya lugha ya mazungumzo imetumika katika kuzungumza kwa kuzingatia miktadha, umri, jinsia na uhusiano | Video na kinyonyi kilichohifadhiwa mitindo mbalimbali ya lugha, michoro | 24 |
| | | (b) Kutumia kwa usahihi ishara zinazoambatana na mazungumzo katika kuwasiliana | **Igizodhima:** Wanafunzi waigize mazungumzo mbalimbali wakizingatia ishara zinazoambatana na mazungumzo | Ishara zinazoambatana na mazungumzo katika kuwasiliana zimetumika kwa usahihi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kuwasiliana kwa njia ya maandishi katika miktadha mbalimbali | (a) Kuandika insha za wasifu na hoja (*za kisanaa na zisizo za kisanaa*) | **Fikiri - Andika-Jozisha - Shirikisha:** Waongoze wanafunzi katika jozi kufikiri kisha waandike mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha za wasifu na hoja na kuwasilisha darasani<br>**Uchunguzi:** Andaa insha kisha waongoze wanafunzi kuchunguza insha za kisanaa na zisizo za kisanaa, wabainishe vipengele vilivyojitokeza katika insha hizo kisha waandike insha | Insha za wasifu na hoja (za kisanaa na zisizo za kisanaa) zimeandikwa | Matini za kuandika, picha na michoro, chati za miundo mbalimbali ya uandishi | 28 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kusikiliza hoja na kuandika kumbukumbu | **Ziara:**<br>Waongoze wanafunzi kushiriki mikutano mbalimbali na kuandika kumbukumbu<br>**Maigizo:**<br>Waongoze wanafunzi kuigiza vikao vyenye kuhusisha hoja mbalimbali | Hoja zimesikilizwa na kumbukumbu zimeandikwa | | |

## Kidato cha III

**Jedwali Na 5:** *Maudhui ya Kidato cha III*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu misingi ya Kiswahili | 1.1 Kukuza uelewa wa sarufi ya Kiswahili | (a) Kuunda maneno kwa njia mbalimbali kutokana na habari alizozisoma au kuzisikiliza (*mf. utohoaji, uradidi, uhulutishaji*) | **Uchunguzi:** Andaa mchoro wenye maneno yaliyoundwa kwa njia mbalimbali kisha waongoze wanafunzi kuchunguza maneno na njia zilizotumika kuyaunda<br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini mbalimbali kisha wabainishe njia zilizotumika kuunda maneno na kuzitumia kuunda maneno mbalimbali | Maneno yameundwa kwa njia mbalimbali za uundaji wa maneno | Picha, kadi za maneno/ tungo, matini za sarufi, kinyonyi kilichohifadhiwa video zenye hoja mbalimbali | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuandika habari kwa kuzingatia maneno yaliyoundwa kwa njia mbalimbali | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini za habari zenye maneno yaliyoundwa kwa kutumia njia mbalimbali kisha waandike habari kwa kutumia maneno yaliyoundwa kwa njia hizo | Habari imeandikwa kwa kuzingatia maneno yaliyoundwa kwa njia mbalimbali | | |
| | | (c) Kujenga hoja za uga mahususi kwa kutumia miundo mbalimbali ya sentensi (*mf. siasa, uchumi, kilimo na biashara*) | **Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kufanya mdahalo kuhusu hoja za uga fulani kwa kutumia miundo mbalimbali ya sentensi | Hoja za uga mahususi zimejengwa kwa kutumia miundo mbalimbali ya sentensi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kusikiliza mazungumzo/ mahojiano katika vyombo vya habari kisha wajenge hoja kwa kutumia miundo mbalimbali ya sentensi kulingana na uga mahususi | | | |
| | | (d) Kuandika matini ndefu na changamani kwa kutumia miundo mbalimbali ya sentensi | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini ndefu na changamani zenye miundo mbalimbali ya sentensi kisha waandike matini ndefu na changamani kwa kutumia miundo mbalimbali ya sentensi | Matini ndefu na changamani zimeandikwa kwa kutumia miundo mbalimbali ya sentensi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumudu lugha ya mazungumzo na ya maandishi | 2.1 Kusikiliza na kuelewa mazungumzo | (a) Kusikiliza habari changamani kitunduizi na kuchangia au kutoa maoni mwafaka | **Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kusikiliza hoja katika habari changamani kitunduizi kisha watoe maoni mwafaka | Habari changamani zimesikilizwa kitunduizi na maoni mwafaka yametolewa | Video na kinyonyi kilichohifadhiwa habari zilizorekodiwa | 10 |
| | | (b) Kusikiliza habari na kuzielezea kwa maneno yake mwenyewe kwa kuzingatia stadi za mawasiliano (*mf. uwazi, ukamilifu wa hoja, usahihi, muwala, uwekevu na staha*) | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusikiliza habari kisha waelezee kwa maneno yao wenyewe kwa kuzingatia stadi za mawasiliano (*mf. uwazi, ukamilifu wa hoja, usahihi, muwala, uwekevu na staha*) | Habari zimesikilizwa na kuelezwa kwa maneno yao wenyewe kwa kuzingatia stadi za mawasiliano | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu | (a) Kusoma matini ndefu changamani na kuelezea kwa maandishi mawazo makuu yaliyomo kwa kuzingatia stadi za mawasiliano (*mf. uwazi, ukamilifu wa hoja, usahihi, muwala, uwekevu na staha* | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini ndefu changamani kisha kuelezea kwa maandishi mawazo makuu yaliyomo kwa kuzingatia stadi za mawasiliano (*mf. uwazi, ukamilifu wa hoja, usahihi, muwala, uwekevu na staha*) | Matini ndefu changamani zimesomwa na kuelezea kwa maandishi mawazo makuu yaliyomo kwa kuzingatia stadi za mawasiliano | Matini changamani za kusoma, kadi za maneno/tungo | 10 |
| | | (b) Kusoma matini ndefu changamani na kutathmini hoja zilizomo | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini ndefu changamani kisha wazitathmini hoja zilizomo | Matini ndefu changamani zimesomwa na hoja zilizomo zimetathminiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 3.1 Kuwasiliana kwa ufasaha kwa njia ya mazungumzo | (a) Kutumia lugha fasaha katika mazungumzo ya hadhara (*mf. mikutano ya hadhara, uwasilishaji mbele ya halaiki na mijadala mbalimbali*) | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kuchunguza mazungumzo mbalimbali ya hadhara kwa kusikiliza ili kubaini lugha fasaha inavyotumika kisha na wao wazungumze kwa kutumia lugha fasaha | Lugha fasaha katika mazungumzo ya hadhara imetumika | Video na kinyonyi kilichohifadhiwa mazungumzo mbalimbali, picha na michoro | 5 |
| | 3.2 Kuwasiliana kwa njia ya maandishi katika miktadha mbalimbali | (a) Kuandika barua na makala za magazetini | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kukusanya barua na makala za magazetini za aina tofauti kisha wabainishe muundo na waandike barua na makala za magazetini | Barua na makala za magazetini zimeandikwa | Matini za kuandika, picha na michoro, chati za miundo mbalimbali ya uandishi | 5 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4.0 Kuthamini kazi za fasihi ya Kiswahili | 4.1 Kukuza uelewa wa misingi ya fasihi ya Kiswahili | (a) Kufafanua dhana ya fasihi na fasihi ya Kiswahili (*maana, aina na dhima*) | **Ramani ya dhana:** Andaa mchoro wa fasihi na fasihi ya Kiswahili. Jaza baadhi ya vipengele na vingine vijazwe na wanafunzi. Kutokana na mchoro huo wanafunzi waeleze maana na aina ya fasihi na fasihi ya Kiswahili | Dhana ya fasihi na fasihi ya Kiswahili imefafanuliwa | Picha, michoro, matini na video zenye kazi za fasihi | 10 |
| | | (b) Kuchambua tanzu za fasihi simulizi na andishi | **Mchezo:** Andika tanzu za fasihi simulizi na andishi kwenye vikaratasi kisha viweke kwenye boksi. Gawa wanafunzi katika makundi mawili ya ushindani yaani kundi A na kundi B ambapo kundi moja litakuwa fasihi simulizi na lingine fasihi andishi. | Tanzu za fasihi simulizi na andishi zimechambuliwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kila kundi litapaswa kuokota vikaratasi kulingana na upande lililopo, kisha kundi zima litapaswa kuandika tanzu walizoziokota kwenye chatipindu halafu wabandike ubaoni. Waongoze wanafunzi kujadiliana kwa pamoja tanzu za fasihi simulizi na andishi<br><br>**Majigambo:**<br>Wape wanafunzi uhusika kutokana na tanzu za fasihi simulizi na andishi kisha kila mhusika kulingana na utanzu alionao ajigambe kwa kuelezea sifa za utanzu huo | | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.2 Kuhakiki kazi za fasihi ya Kiswahili | (a) Kujadili dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi (*maana ya uhakiki, mhakiki na sifa za mhakiki*) | **Bunguabongo:** Waongoze wanafunzi kubungua bongo kuhusu maana ya uhakiki na mhakiki<br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi vidogovidogo kujadiliana kuhusu sifa za mhakiki | Dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi imejadiliwa | Matini zenye kazi za fasihi, michoro na vielelezo | 25 |
| | | (b) Kufafanua misingi ya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi na fasihi andishi (*vipengele vya fani na maudhui*) | **Uchunguzi:** Andaa kazi za fasihi simulizi na andishi kisha waongoze wanafunzi kuzihakiki na kueleza misingi ya uhakiki<br>**Maigizo:** Waongoze wanafunzi kuigiza kisa fulani kisha wabainishe vipengele vya fani na maudhui vilivyojitokeza | Misingi ya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi na andishi imefafanuliwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Hadithi:**<br>Waongoze wanafunzi kusimulia hadithi kisha wabainishe vipengele vya fani na maudhui vilivyojitokeza | | | |
| | | (c) Kuhakiki fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi (*mashairi na maigizo*) | **Uchambuzi wa matini:**<br>Waongoze wanafunzi kusoma matini mbalimbali zenye mashairi kisha wachambue matini hizo kwa kuangalia fani na maudhui yake<br><br>**Uchunguzi:**<br>Waongoze wanafunzi kuangalia video zenye maigizo au mashairi kisha waeleze mambo waliyobaini | Fani na maudhui katika kazi za fasihi simulizi zimehakikiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Maigizo:**<br>Waongoze wanafunzi kuigiza matukio au visa mbalimbali kwa kuzingatia vipengele vya fani na maudhui | | | |
| | | (d) Kuhakiki fani na maudhui katika tamthiliya | **Uchambuzi wa matini:**<br>Waongoze wanafunzi kusoma tamthiliya kisha wachambue vipengele vya fani na maudhui<br><br>**Majadiliano:**<br>Waongoze wanafunzi kuangalia video zenye tamthiliya kisha wachambue vipengele vya fani na maudhui katika vikundi | Fani na maudhui katika tamthiliya vimehakikiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kutathmini namna maudhui ya kazi alizozihakiki yanavyosadifu jamii inayomzunguka | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini kisha kutathmini namna maudhui ya kazi walizozihakiki yanavyosadifu jamii inayowazunguka<br>**Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kujibu maswali kuhusu namna maudhui ya kazi walizozihakiki yanavyosadifu jamii inayomzunguka<br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili namna maudhui ya kazi walizozihakiki yanavyosadifu jamii inayomzunguka | Maudhui ya kazi alizozihakiki yametathminiwa kwa kuhusianisha na namna yanavyosadifu jamii inayomzunguka | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.3 Kubuni kazi za fasihi ya Kiswahili | (a) Kujadili kanuni za utunzi wa nyimbo, ngonjera na maigizo | **Nyimbo:** Waongoze wanafunzi kuimba nyimbo mbalimbali kisha wajadili kanuni zilizotumika kutunga tanzu hizo<br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini mbalimbali zenye nyimbo, ngonjera na maigizo kisha wajadiliane kanuni zilizotumika kutunga tanzu hizo<br>**Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kuangalia video zenye nyimbo, ngonjera na maigizo mbalimbali kisha waeleze waliyoyabaini | Kanuni za utunzi wa nyimbo, ngonjera na maigizo zimejadiliwa | Matini zenye nyimbo, ngonjera, maleba, vifaa vya kuigizia | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kutunga nyimbo, ngonjera na maigizo | **Oneshombinu:** Waongoze wanafunzi kuangalia na kusikiliza nyimbo, ngonjera na maigizo kwa kutumia vifaa vya TEHAMA kisha wabaini kanuni za utunzi na kutunga nyimbo, ngonjera na maigizo | Nyimbo, ngonjera na maigizo vimetungwa | | |
| | | (c) Kuimba nyimbo na kutamba ngonjera | **Nyimbo:** Waongoze wanafunzi kuimba nyimbo<br>**Majibizano:** Waongoze wanafunzi kutamba ngonjera | Nyimbo zimeimbwa na ngonjera zimetambwa | | |
| | | (d) Kuigiza maigizo | **Maigizo:** Waongoze wanafunzi kuigiza | Maigizo yameigizwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5.0 Kutoa huduma ya lugha ya Kiswahili katika jamii | 5.1 Kufanya tafsiri sahili katika lugha ya Kiswahili | (a) Kujadili dhana, misingi, kanuni, na hatua za tafsiri | **Bunguabongo:** Waongoze wanafunzi kubunguabongo kuhusu maana ya tafsiri<br>**Uchambuzi wa matini:** Andaa matini iliyohawilishwa pamoja na matini chanzi yake, waongoze wanafunzi kuzisoma na kuzichambua kisha wajadili dhana, misingi, kanuni, na hatua za tafsiri<br>**Kualika mgeni:** Alika mgeni mwenye taaluma ya tafsiri ili kushirikisha uzoefu wa tafsiri | Dhana, misingi, kanuni, na hatua za tafsiri zimejadiliwa | Matini mbalimbali, orodha ya istilahi, orodha ya vifupisho | 15 |
| | | (b) Kutafsiri matini fupi sahili | **Kazimradi:** Andaa matini chanzi za Kiingereza kisha wape wanafunzi wakazitafsiri katika Kiswahili na kuziwasilisha darasani | Matini fupi sahili zimetafsiriwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kutatua changamoto zinazojitokeza katika kutafsiri matini | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kutafsiri matini fupi sahili kisha kutatua changamoto zinazojitokeza | Changamoto zinazojitokeza katika kutafsiri matini zimetatuliwa | | |
| | 5.2 Kuhariri matini mbalimbali za Kiswahili | (a) Kujadili dhana, kanuni na misingi ya uhariri | **Bunguabongo:** Waongoze wanafunzi kubungua bongo kuhusu dhana, kanuni, na misingi ya uhariri<br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kusoma nakala ya matini ambayo haijahaririwa na iliyohaririwa, kisha wabainishe mambo waliyoyaona | Dhana, kanuni na misingi ya uhariri imejadiliwa | Matini mbalimbali, kamusi | 20 |
| | | (b) Kuhariri matini fupi za Kiswahili | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kuhariri matini fupi | Matini fupi za Kiswahili zimehaririwa | | |

## Kidato cha IV

**Jedwali Na 6:** *Maudhui ya Kidato cha IV*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kuwasiliana kwa ufasaha kwa njia ya mazungumzo | (a) Kuigiza usaili kwa kuzungumza na kuandika | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kujibu maswali kuhusu usaili<br>**Oneshombinu:** Waongoze wanafunzi kuigiza usaili wa kuzungumza na kuandika | Usaili umeigizwa kwa kuzungumza na kuandika | Nakala za wasifukazi na tawasifu | 8 |
| | 1.2 Kuwasiliana kwa njia ya maandishi katika miktadha mbalimbali | (a) Kuandika wasifukazi na tawasifu | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini zenye wasifukazi na tawasifu kisha waeleze vitu muhimu walivyovibaini | Wasifukazi na tawasifu zimeandikwa | Nakala za wasifukazi na tawasifu | 8 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kukusanya maandiko mbalimbali yenye wasifukazi na tawasifu, wachunguze maandiko hayo kisha waandike wasifukazi na tawasifu | | | |
| 2.0 Kuthamini kazi za fasihi ya Kiswahili | 2.1 Kuhakiki kazi za fasihi ya Kiswahili | (a) Kujadili dhana ya mashairi andishi | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini zenye mashairi andishi kisha waeleze dhana ya mashairi andishi | Dhana ya mashairi andishi imeelezwa | Diwani mbalimbali na matini zenye mashairi, riwaya, tamthiliya, chati ya fani na maudhui | 28 |
| | | (b) Kuhakiki fani na maudhui katika mashairi andishi | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini zenye mashairi andishi kisha wachambue vipengele vya fani na maudhui vya utanzu huo | Fani na maudhui katika mashairi andishi vimehakikiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuhakiki fani na maudhui katika riwaya | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kusoma riwaya teule kisha wabainishe vipengele vya fani na maudhui | Fani na maudhui katika riwaya vimehakikiwa | | |
| | | (d) Kuhusianisha kazi za fasihi na maisha halisi | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadiliana namna ujumbe walioupata katika kazi walizozihakiki unavyofungamana na maisha halisi | Kazi za fasihi zimehusanishwa na maisha halisi | | |
| | 2.2 Kubuni kazi za fasihi ya Kiswahili | (a) Kujadili kanuni za utunzi wa hadithi fupi simulizi na andishi | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusimuliana hadithi mbalimbali kisha wajadili kanuni za utunzi | Kanuni za utunzi wa hadithi simulizi na hadithi fupi zimejadiliwa | Matini zenye hadithi, kamusi | 32 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini zenye hadithi fupi kisha wabainishe mambo yaliyozingatiwa katika hadithi hizo | | | |
| | | (b) Kutunga hadithi fupi simulizi na andishi | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kutunga hadithi fupi na hadithi simulizi | Hadithi fupi na hadithi simulizi zimetungwa | | |
| | | (c) Kutamba hadithi | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kutamba hadithi simulizi<br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini za hadithi fupi kisha watambe | Hadithi zimetambwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kutoa huduma ya lugha ya Kiswahili katika jamii | 3.1 Kufanya tafsiri sahili katika lugha ya Kiswahili | (a) Kutafsiri matini ndefu sahili | **Kazimradi:** Waweke wanafunzi katika vikundi vidogovidogo, wape matini wazitafsiri katika muda maalumu kisha waziwasilishe darasani | Matini ndefu sahili zimetafsiriwa | Matini mbalimbali, kamusi, orodha ya vifupisho na orodha ya istilahi | 20 |
| | | (b) Kutathmini matini zilizotafsiriwa | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini zilizotafsiriwa, wabainishe makosa yaliyomo, kisha wapendekeze tafsiri sahihi katika vipengele vyenye makosa | Matini zilizotafsiriwa zimetathminiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kuhariri matini mbalimbali za Kiswahili | (a) Kuhariri matini ndefu za Kiswahili | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kuchambua matini mbalimbali kisha wabainishe makosa ya kiuandishi, na kuzihariri matini hizo | Matini ndefu za Kiswahili zimehaririwa | Matini mbalimbali, kamusi | 20 |
| | | (b) Kutathmini matini zilizohaririwa | **Kazimradi:** Wape wanafunzi matini zilizohaririwa, wazisome na kuzitathimini katika muda maalumu kisha waziwasilishe darasani | Matini zilizohaririwa zimetathminiwa | | |
| | 3.3 Kufanya ukalimani sahili kwa lugha ya Kiswahili | (a) Kujadili dhana na misingi ya ukalimani | **Bunguabongo:** Waongoze wanafunzi kubunguabongo kuhusu maana na istilahi zinazotokana na fasili ya ukalimani | Dhana na misingi ya ukalimani imejadiliwa | Video zenye maudhui ya ukalimani | 24 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili misingi ya ukalimani | | | |
| | | (b) Kueleza stadi muhimu katika ukalimani | **Maswali na majibu:** Wanafunzi wasikilize ukalimani, kisha mwalimu awaulize na kuwaongoza kujibu maswali kuhusu stadi muhimu za ukalimani | Stadi muhimu katika ukalimani zimeelezwa | | |
| | | (c) Kukalimani mazungumzo mafupi na sahili katika miktadha mbalimbali | **Igizodhima:** Waongoze wanafunzi kukalimani mazungumzo mafupi na sahili katika miktadha mbalimbali | Mazungumzo mafupi na sahili yamekalimaniwa katika miktadha mbalimbali | | |

## Bibliografia


Baraza la Kiswahili la Taifa. (2013). *Mwongozo wa waandishi wa Kiswahili sanifu.* BAKITA.

Chomi, W. E. ( 2013). *Kitangulizi cha mofolojia ya Kiswahili.* TUKI.

Habwe, J., & Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili.* Phoenix Publishers Ltd.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., na Msanjila, Y. P. (2003). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu.* TUKI.

King'ei, K. (2014). *Taaluma ya uandishi.* The Jomo Kenyatta Foundation.

Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi.* Mture Educational Publishers Ltd.

Massamba, D. P. B., Kihore. Y. M., na Hokororo, J. I. (2012). *Sarufi miundo ya Lugha ya Kiswahili sanifu: Sekondari na vyuo. (SAMIKISA).* TUKI.

Mgullu, R. (2001). *Mtalaa wa isimu: Fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili.* Longhorn Publishers Ltd.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki.* EAEP.

Mwansoko H. J. M., Mekacha, R. D. K., Masoko, D. L. W. na Mtesigwa, P. C. K. (2015). *Kitangulizi cha tafsiri: Nadharia na mbinu.* TUKI.

Nkwera, F. (1978). *Sarufi na fasihi, sekondari na vyuo.* Tanzania Publishing House.

Senkoro, F. (1987). *Fasihi na jamii.* Press and Publicity Centre.

*Senkoro, F. (1988). Ushairi: Nadharia na tahakiki.* Dar es Salaam University Press.

Senkoro, F. (2011). *Fasihi.* KAUTTU.